



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



07 Desemba, 2021

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI:

KUUNDWA KWA TIMU MBILI ZA WATAALAM YA UTEKELEZAJI WA SHERIA NDOGO YA MAPATO KWA WASIOLIPA KODI NA MAPATO YA MANISPAA NA TIMU YA UKUSANYAJI WA MAPATO MTA A KWA MTA A.

Ili kufikia malengo ya kukusanya mapato ya ndani ya Tshs. **49,413,888,000**, ifikapo **Juni 30,2022**, Manispaa ya Kinondoni imeamu kuunda Timu mbili ili kuwezesha Malengo hayo kufikiwa kama ifuatavyo:-

1. Timu ya Wataalamu kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria ndogo ya Mapato kwa wanaokwepa kulipa au wanaokadi kulipa ambayo itafanya kazi ya kuwafikisha katika vyombo vya sheria wadaiwa sugu wanaokwepa au kukaidi kulipa kodi. Timu hii itakuwa na wahasibu wawili na wanasheria wawili.
2. Timu ya ukusanyaji wa Mapato Mtaa kwa Mtaa, itakayopita Mtaa kwa Mtaa kukusanya mapato kwenye vyanzo 11 vya Mapato ya ndani ya Manispaa. Timu hii itakuwa na watumishi 19 wa Idara na vitengo mbalimbali.

Timu zote mbili zinaanza kazi leo **Jumatano tarehe 08/12/2021**.

Vyanzo vya Mapato vitakavyopitiwa na kukusanywa ni kama ifuatavyo:-

- Ushuru wa huduma
- Lesseni za Biashara
- Uwekezaji
- Ushuru wa Madini
- Ukodishaji Mabanda kwenye Masoko
- Ushuru wa vizimba kwenye masoko
- Ada ya huduma ya vyoo
- Vibali vya ujenzi na Ushuru wa kuzingira
- Ukodishaji wa mali za Manispaa
- Usafi kata (Ada ya usafi).

Hivyo Manispaa ya Kinondoni inawataka wadaiwa wote sugu kutoa ushirikiano kwa kutekeleza jukumu lao la kulipa na kuwasiliana na Ofisi ya Mkurugenzi.

Aidha ninawaasa viongozi wote wa Manispaa kuanzia ngazi ya Mtaa hadi Manispaa kutoa ushirikiano kwa timu hizi mbili ili tuweze kufikia malengo ya kukusanya mapato na kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

“LIPA KODI KWA MAENDELEO YA MANISPAA”

Imetolewa na:-

Mhe: Songoro Mnyonge
Mstahiki Meya wa Manispaa
MANISPAA YA KINONDONI